AHADI>> Nitakuwa balozi mzuri kwa vijana wenzangu

# DART yarejesha mwendokasi Kimara, Gerezani, Kivukoni

**Na ELIZABETH JOHN**

MAMLAKA ya Usafiri wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART), imesema imerejesha huduma ya mabasi hayo kati ya Kimara-Gerezani na Kimara-Kivukoni.

Usafiri katika njia hizo ulisimama kutokana na uharibifu wa miundombinu yake vikiwemo vituo katika vurugu zilizotokea siku ya uchaguzi na baada ya hapo.

Aidha, DART imesema inaendelea kukarabati miundombinu hiyo ikiwemo mifumo ya kielektroniki ya kukusanya nauli katika maeneo mbalimbali.

Mkuu wa Mawasiliano wa DART, William Gatambi, alisema vurugu zilizotokea siku ya uchaguzi mkuu, Oktoba 29, mwaka huu, zilisababisha uharibifu mkubwa uliosababisha usitishaji wa huduma hizo.

Alisema juhudi za Serikali na wadau zimefanikiwa kurejesha huduma katika vituo vilivyo salama vikiwemo Ubungo Maji, Urafiki, Fire, DIT, Kisutu, Posta, Kivukoni na Gerezani.

"Kwa sasa, abiria wanaruhusiwa kushuka katika vituo vyote kuanzia Ubungo Maji kwenda Kivukoni au Gerezaji, lakini hawataruhusiwa kupanda kutokana na uharibifu katika maeneo mengine. Tunaendelea na kazi ya kurekebisha mifumo na miundombinu ili huduma irejee kikamilifu," alisema Gatambi.

Aidha, alieleza ukarabati katika maeneo mengine kama Ubungo–Kimara na Ubungo–Morocco, unaendelea kwa awamu, na Serikali itahakikisha miundombinu yote inakamilika kwa usalama na ufanisi.

Mkazi wa Shekilango, Nickson Jumanne, aliitaka jamii kutunza miundombinu ya umma kuepuka madhara yanayotokana na uharibifu wa mali za Serikali.

"Huduma ya mwendokasi ilikuwa ni rahisi kwetu, lakini sasa tunakutana na changamoto kubwa. Tunaiomba jamii itunze miundombinu hii kuepuka hasara zaidi," alisema.

Kwa upande wake, Mwajuma Hussein, mkazi wa Ubungo, aliiomba DART kurejeshwa matumizi ya tiketi za karatasi na kadi maalumu za kielektroniki, wakieleza mfumo wa kadi umeleta changamoto za upatikanaji wa kadi na baadhi ya abiria wamekuwa wakikumbana na ugumu wa kutumia programu za simu.

Hatua hizi zinafuatia agizo la Waziri Mkuu, Dk. Mwigulu Nchemba, alilotoa akitaka marekebisho ya haraka katika miundombinu ya usafiri wa mwendokasi, kurejesha huduma kikamilifu na kudhibiti changamoto zinazojitokeza.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, Profesa Riziki Shemdoe, alitoa siku nne kuhakikisha huduma inarejea katika maeneo yaliyosimama kutokana na vurugu hizo.

# MWANANCHI

TANZANIA

Alhamisi, Desemba 4, 2025 MWANANCHI.CO.TZ ISSN 0856-7573 NA. 9244 BEI: TSH 1,000, KSH 60







## Kauli ya Niffer baada ya siku 38 mahabusu

Mahakama imemwachia huru mfanyabiashara wa vipodozi, Jenifer... UK6








# Kimbembe cha usafiri mikoani

**Mamia ya abiria kutoka Dar wafurika vituoni kusaka usafiri, Taboa yatoa angalizo. Yaliyotokea Oktoba 29, hofu ya Desemba 9 vyatajwa**

HABARI UK 2



"Ni kweli kuna hofu fulani ya kile kilichotokea Oktoba 29 Dar es Salaam. Sasa baadhi wanarudi mapema kabla ya Desemba 7, japo Rais ametoa hakikisho la usalama, bado kuna hofu." Khalid Shekoloa

## Polisi yataja mambo 12 kujihadhari Desemba 9

Jeshi la Polisi nchini limetaja mambo 12 linayodai yanaendelea kupangwa mitandaoni kuelekea Desemba 9, mwaka huu, huku likiwataka wanaopanga na kuhamasisha vitendo vya uvunjifu wa amani siku hiyo kuachana navyo, la sivyo watashughulikiwa.

Polisi wamebainisha... UK4



David Misime, Msemaji wa Jeshi la Polisi

## Wapenzi wadakwa na dawa hatari, mali za Sh3 bil zataifishwa



HABARI UK 3

## Njia za kujitegemea bila misaada ya nje

Tanzania inaweza kujitegemea kwa kutumia makusanyo ya ndani yanayotokana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na yale yasiyo ya kikodi ... UK12

CamScanner

USAFIRI WA UMMA

# Kimbembe cha usafiri

Waandishi Wetu, Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

**Dar es Salaam.** Licha ya Desemba kuwa na historia ya changamoto ya usafiri kutoka Dar es Salaam kwenda mikoani, mwaka huu imekuwa zaidi ya kawaida, kwani idadi kubwa ya abiria imeshuhudiwa, huku baadhi wakikwama kusafiri.

Kwa mujibu wa watoa huduma za usafiri wa mikoani, idadi ya abiria wanaosafiri sasa kutoka Dar es Salaam kwenda mikoani ni zaidi ya kawaida. Hali kama hiyo mara nyingi hushuhudiwa kuanzia Desemba 20.

Wakizungumza jana, watoa huduma hao walisema mwaka huu, mafuriko ya abiria yameanza mwishoni mwa Novemba na mwanzoni mwa Desemba, hali inayozua swali, kwanini mapema zaidi ya kawaida?

Wapo wanaohusisha hali hiyo na tishio la kiusalama katika Jiji la Dar es Salaam, eneo lililopangwa kuwa kitovu cha maandamano ya Desemba 9, kwa mujibu wa taarifa katika mitandao ya kijamii.

Hofu hiyo inajengwa na kumbukumbu za maisha magumu waliyopitia wakazi wa Dar es Salaam wakati wa maandamano yaliyozaa vurugu ya Oktoba 29, yaliyosababisha vifo, majeruhi, na uharibifu wa mali za umma na binafsi.

Katika vurugu hizo, Jeshi la Polisi lilitoa amri ya wananchi kutotoka nje kuanzia saa 12 jioni, iliyodumu kwa takriban siku tano. Baadhi yao walitaabika kwa kukosa chakula na huduma nyingine muhimu.

Hata hivyo, Desemba 2, Rais Samia Suluhu Hassan alitangaza hakikisho la usalama katika jiji hilo na maeneo mengine, akisema Serikali imejipanga kudhibiti matukio hayo wakati wowote.

### Hali ya sasa

Mmoja wa wasafiri, Daniel Michael, aliyekuwa anatokea Tanga kuelekea Moshi mjini, alisema ameshuhudia magari mengi binafsi yakiingia mkoani Kilimanjaro, jambo ambalo si la kawaida kwa tarehe hizo.

"Tunajua Desemba hii wakazi wengi wa Kilimanjaro, hususan Wachaga, hurudi kwao kwa ajili ya sikukuu za mwisho wa mwaka, lakini si kwa tarehe hizi, ni kuanzia katikati ya Desemba. Sijui kwa nini safari hii wanawahi hivi," alisema.

Katika Njiapanda ya Himo kuanzia saa 10 alasiri, kumeonekana magari yenye namba mpya (E), yaliyotokea Tanga au Dar es Salaam, yakielekea maeneo ya Mwika, Marangu, Kilema, Wilaya ya Moshi na Rombo.

Mbali na Njiapanda ya Himo, katikati ya Mji wa Moshi kumeanza kuonekana magari mageni ambayo kwa kawaida huonekana kuanzia katikati ya Desemba hadi Januari 3, na baadhi ni wageni wa barabara.

Maria Mageni alitarajia kusafiri na familia yake kuanzia Desemba 15 kwenda Magu, mkoani Mwanza, lakini mumewe amelazimika kubaki Dar es Salaam baada ya kukosa tiketi, ikidaiwa zimeisha.

Safari yake inasababishwa na kile alichoeleza kuwa amejifunza kwa matukio ya Oktoba 29, hivyo anaondoka mapema ili kuepuka hali zinazotarajiwa kuanza Desemba 9.

"Nilipanga kuondoka Desemba 15, lakini kutokana na funzo nililolipata Oktoba 29, nilijifungia muda wote. Kinachosemekana kinaenda kutokea kimeniambia niwahi kijijini," alisema.

Maisha yake wakati wa vurugu hizo, alisema yalikuwa magumu kwa kuwa alikosa hata chakula na kulazimika kusaidiwa na wapangaji.

"Mazingira ya Dar es Salaam na kinachosemekana kinapangwa kutokea hayawezekani. Ni bora niwahi kijijini kwa ndugu zangu na familia," alisema Maria.

Kama ilivyo kwa Maria, Shadrack Mwakareli naye amefungasha virago kulikimbia Jiji la Dar es Salaam kwenda kijijini Tukuyu, mkoani Mbeya, akisema ni salama zaidi.

"Kupata chakula Dar es Salaam si rahisi. Hadi mazingira yakichafuka unaweza kufia ndani. Maandamano haya yanayosemekana kuanza Desemba 9 hayana ukomo. Ni bora nijilinde mapema," alisema Mwakareli.

Hadi anapoamua kusafiri, alisema ameshapigiwa simu kadhaa na ndugu zake kutoka kijijini, wakimtaka aende kwa maslahi ya usalama wake.

Hata hivyo, malengo ya Mwakareli yanakumbwa na kikwazo, baada ya kukuta mabasi yamejaa na yaliyopo wamepandisha bei kupitiliza.

"Nimefika hapa alfajiri lakini bado sijapata usafiri. Changamoto ni bei za tiketi kupanda sana, lakini hakuna namna, uhai ni muhimu zaidi," alisema.

Shida ya usafiri ilimkabili pia Neema Konzo, aliyesema alikwenda Kituo cha Mabasi cha Magufuli, Dar es Salaam, Jumatatu, akakosa tiketi na kulazimika kukata ya kusafiri Alhamisi.

"Nimenunua tiketi Jumatatu, Desemba mosi. Nilifika Mbezi asubuhi kwa lengo la kusafiri lakini sikupata tiketi, ilinibidi nikate kwanza nikapata ya siku ya Alhamisi, hivyo nilirudi nyumbani kusubiri tarehe ya safari," alisema Neema, aliyekuwa akisafiri kwenda Njombe.

Joseph Rukamba, anayesafiri kwenda Bukoba, alisema: "Nimefika hapa tangu alfajiri lakini tiketi zimeisha. Nimeambiwa zimejaa hadi Desemba 8. Sitaweza kubaki Dar es Salaam, nitatafuta hata usafiri wa kuunga."

Alisema matarajio yake ni kufika nyumbani kabla ya Desemba 8, hivyo hataweza kusubiri kwani wazazi na ndugu zake wanampigia simu mara nyingi kumwomba arudi kijijini.

Katika hatua nyingine, Msemaji wa Jeshi la Polisi, David Misime, aliwataka wananchi watakaosafiri msimu wa sikukuu kuhakikisha wanaacha waangalizi au walinzi wa maisha na mali zao.

"Vilevile wazingatie sheria za usalama barabarani na kufuata ishara zilizopo ili kuepuka ajali," alisema.

> **USULI**
>
> **Oktoba 29, makundi ya vijana maarufu Gen Z, walifanya maandamano yaliyozaa vurugu mikoa mbalimbali nchini.**
>
> **Hatua hiyo ilisababisha uharibifu wa miundombinu, mali za umma, za binafsi, vifo vya watu na majeruhi.**
>
> **Kutokana na matukio hayo, Rais Samia, Novemba 18, alizindua tume ya kuchunguza chanzo cha matukio hayo inayoongozwa na Jaji Mkuu wa Tanzania mstaafu, Mohamed Chande Othman.**

### Uchunguzi wa Mwananchi

*Mwananchi* ilishuhudia idadi kubwa ya watu katika Kituo cha Mabasi cha Magufuli wakizunguka kutafuta tiketi za kusafiri. Waliokuwa wamekalia na wengine kulala mabegi yao, huku watoto wakiwa chini, baadhi wakisubiri hatima ya kusafiri.

Mbali na hilo, Desemba 3, saa 10:00 jioni, *Mwananchi* iliingia katika tovuti za ukatishaji tiketi za kampuni kadhaa za mabasi zinazofanya safari za mikoani na kushuhudia yakiwa yamejaa.

Katika kampuni ya mabasi ya BM Coach kwa safari ya mkoani Arusha, Desemba 4, mabasi matano kati ya 10 yalijaa, mawili yakiwa na nafasi chache, na lingine la abiria wa hadhi maalumu viti 38.

Kwa kampuni ya mabasi ya Ally's Star kwa safari ya mkoani Mwanza, Desemba 4, kati ya mabasi manne, mawili yalijaa na moja lilibaki na viti vinne, lingine la hadhi maalumu viti 38.

Kampuni ya mabasi ya Abood kwa safari ya mkoani Morogoro Desemba 4, mfumo wake umeonyesha 'busy', ukimaanisha unatumika kwa wengi.

### Watoa huduma

Mmoja wa wakatisha tiketi wa kampuni moja ya mabasi (jina limehifadhiwa) alikiri kuwapo kwa ongezeko la wasafiri na hivyo kusababisha ugumu wa usafiri.

"Sababu mojawapo ni tishio la maandamano ya Gen Z Desemba 9. Baadhi wameona ni bora waondoke Dar es Salaam mapema kurudi Kilimanjaro, hasa ikizingatiwa mkoa wetu hauna historia ya vurugu. Huwa ni tulivu," alisema.

Kutokana na wingi wa abiria, alisema kampuni yao ina mabasi sita yanayofanya safari za mikoani, yote yamejaa, na wameongeza moja la ziada.

Mmiliki wa kampuni ya mabasi ya Kapricon, George Mberesero, alisema mbali na hofu ya maandamano, ugumu wa usafiri unasababishwa pia na wanafunzi wanaohitaji kurudi nyumbani baada ya kufunga shule.

Mwenyekiti wa Umoja wa Mabalozi wa Usalama Barabarani Tanzania (RSA), Mkoa wa Kilimanjaro, Khalid Shekoloa, amekiri ongezeko la abiria wanaotoka Dar es Salaam kwenda Kilimanjaro, akisema baadhi yao ni kwa hofu ya Desemba 9.

"Ni kweli kuna hofu fulani ya kile kilichotokea Oktoba 29 Dar es Salaam. Sasa baadhi wanarudi mapema kabla ya Desemba 7, japo Rais ametoa hakikisho la usalama, bado kuna hofu," alisema.

Pamoja na hofu, Shekoloa alisema ongezeko la abiria limechangiwa pia na wanafunzi wanaorudi makwao, akisisitiza kuwa baadhi ya wenyeji wa Kilimanjaro wanarudi mapema kwani mkoa wao ni salama.

"Kule (Dar) wana kumbukumbu ya Oktoba 29, watu walifungiwa ndani, maduka yakafungwa kwa siku takriban tano. Mkoa wa Kilimanjaro ni shwari, hapakuwa na vurugu hizo, ni vija na wachache walijaribu Polis ikawadhibiti," alisema.

### Taboa

Msemaji wa Chama cha Wami liki wa Mabasi Tanzania (Taboa Mustapha Mwalongo, alisem kuanzia Desemba mosi, idadi y abiria wanaohitaji kusafiri kuto ka Dar es Salaam imeongezek kwa kasi.

Kuhusu ukaguzi wa tiket Mwalongo amewataka abir kununua tiketi katika vituo ra mi au kwa mawakala waliotar bulika ili kuepuka vitendo v utapeli kutokana na msongam no.

"Nawasihi abiria kuhakikisl wanakata tiketi katika vituo ra mi au kupitia mawakala war otambulika, ili kuepuka usumb fu na hasara," alisema.

Alisema wamiliki wa mab kuongeza safari ili wajitah kusafirisha abiria wote, lak ikiwa idadi itazidi, wataom vibali vya kuongeza mabasi ku ka Mamlaka ya Usafiri Ardh (Latra).




Abiria wakiwa eneo la Shekilango wakisubiri kupanda mabasi yaendayo mikoani, kama walivyokutwa na mpigapicha wetu jana. Picha


## Uapisho Mwenyekiti mpya Halmashauri wasitishwa ghafla, mvutano waibuka

Uk. 3



## Vijana wa Kitanzania walengwa uhalifu wa mtandao Myanmar

HABARI UK. 5




# Nipashe

Alhamisi Desemba 4, 2025 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0582240

epaper.ippmedia.com / www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII



Guardian

GAZETI BORA TANZANIA

SUPERBRAND MARA 11 MFULULIZO



URITHI WA UBORA, NA SAFARI YA MAFANIKIO


## KUELEKEA DES 9:

# Mitaani kulivyobadilika

Idadi ya wanaoondoka Dar yashtua, wanajeshi watanda 'kona muhimu', Polisi yataja mbinu za waandamanaji, Jumuiya ya Maridhiano yadai uponyaji Taifa...

HABARI UK. 2,3



Baadhi ya abiria waliokuwa katika Stendi ya Magufuli jana



"Wengine wameapa kuwa watakaoandamana wasithubutu kufika kwenye maeneo yao. Hayo yote yanaashiria wazi dhamira ya kuleta madhara makubwa,"
DCP David Misine

"Hisia hizi zikikolezwa zinaweza kuzaa mgawanyiko mkubwa. Taifa linahitaji uponyaji wa pamoja. Jamii ijifunze kutoa msamaha. Kutosamehe ni mzigo mzito unaoumiza mtu binafsi na taifa,"
Shekhe Dk. Alhad Salum

"Wingi wa abiria wa mabasi safari hii umechangiwa na sababu mbili: msimu wa likizo na hofu ya maandamano yaliyopangwa kufanywa Desemba 9. Katibu Mkuu wa TABOA, Priscus Joseph

## Mali za bilioni 3.3/- zataifishwa kisheria

Ni zao la 'unga', zimo 'apartments', viwanja vya 'uzunguni' na magari, vilimilikiwa na watu wawili...

Uk. 4



Kamishna Jenerali wa DCEA, Aretas Lyimo

## Hatimaye Niffer na Chavala waachiwa huru uhaini Okt. 29

HABARI UK. 5



Mfanyabiashara Jennifer Jovin, maarufu Niffer (kulia), aliyekuwa akikabiliwa na mashtaka ya uhaini, akilakiwa na mama yake mzazi, Mwanaisha Isack baada ya kuachiwa huru katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana. PICHA: IMANI NATHANIEL



## Aliyelipwa milioni 1.5/- aende kuua ahukumiwa kifo cha kunyongwa

HABARI UK. 7

MAANDAMANO

## KUELEKEA DES 9:

# Mitaani kulivyobadilika

Na Waandishi Wetu

HOFU ya maandamano yanayoratibiwa kupitia mitandao ya kijamii kwa ajili ya Desemba 9 imeanza kuonekana wazi jijini Dar es Salaam:

Baadhi ya wakazi wa jiji hilo la kibiashara wameanza kuondoka mapema mjini kuelekea vijijini, huku wengine wakihaha kununua chakula cha kutosha ili kujikinga na madhara yoyote yanayoweza kujitokeza.

Ufuatiliaji wa Nipashe katika masoko na maeneo ya biashara umebaini kuwa wananchi wengi wanakumbuka machungu ya yaliyotokea Oktoba 29, ambapo bidhaa zilipanda bei na baadhi ya watu kushindwa kutoka nje kwa siku kadhaa. Safari hii, wengi wanataka kujihami mapema.



Mwenyekiti wa Machifu wa jiji la Mbeya, Rocket Mwashinga (kushoto), akizungumza na wandishi wa habari, jijini humo juzi, akiwataka vijana wasikubali kurubuniwa na kushiriki maandamano, kutokana tetesi zinazosambaa kupitia mitandao ya kijamii. PICHA: NEBART MSOKWA

Irene Mtandi, mkazi wa Mwananyamala, alikutwa na waandishi wa habari hii sokoni Mapinduzi jana mchana akinunua chakula cha akiba. Alisema alijifunza kutokana na maumivu yaliyopita.

"Tulipata shida sana... tulifika hatua ya kulala njaa kwa sababu tulikuwa hatujaweka akiba. Sasa ninataka nijihami," alisema.

Katika soko la Tandale, Juma Mteite alieleza kuwa baa la Oktoba 29 halipaswi kuwaamsha wananchi; utaratibu wa kuwa na akiba unapaswa kuwa wa kudumu.

"Hata kama si maandamano, linaweza kutokea janga lingine. Ni busara kuwa na chakula nyumbani," alisema.

Kwa upande wa wauzaji, bidhaa zinazouzwa kwa kasi zaidi ni mchele, unga, tambi, maharage, nyanya, viazi na mikate, huku wengine wakisema mahitaji yameongezeka ghafla.

Kutokana na kiwewe cha awali, baadhi ya wakazi wameomba serikali kuhakikisha siku ya maandamano inapita kwa amani ili kuepusha uharibifu wa mali kama uliojitokeza huko nyuma.

Rais Samia Suluhu Hassan alitoa kauli juzi mbele ya wazee wa Dar es Salaam, akiwatoa hofu wananchi na kusisitiza kuwa serikali iko tayari na imejipanga.

### STENDI YA MAGUFULI

Katika Kituo Kikuu cha Mabasi cha Magufuli-Mbezi, Nipashe ilishuhudia abiria wengi wakiharakisha safari zao wakiamini vijijini kutakuwa na utulivu zaidi.

Munira Maliki, mmoja wa abiria waliokutwa kituoni huko, alisema: "Ni bora nikae Tanga. Mjini hatujui kitakachotokea. Yale ya mwanzo yalitukuta ghafla."

Wengine kama Godfrey Polycarp, aliyekuwa akielekea Moshi, walisema safari zao za mapema zimechangiwa na hofu ya kisichoeleweka.

"Mimi huwa ninaondoka tarehe 20 Desemba, lakini safari hii nimeharakisha. Wachaga wengi pia wameshaanza kuondoka."

Hata hivyo, baadhi yao walikiri kuwa hata vijijini hakukuwa shwari wakati wa vurugu za nyuma, lakini wanaona angalau kuna ahueni ya kujiepusha na misongamano ya mijini.

Katibu Mkuu wa TABOA, Priscus Joseph, alisema jana kuwa wingi wa abiria safari hii umechangiwa na sababu mbili: msimu wa likizo na hofu ya maandamano.

Kondakta wa Kampuni ya Tilisho, Fatuma Ally, aliyepata tuzo ya kuwa kondakta bora wa mwaka hivi karibuni, tuzo zilizotolewa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), alisema safari zimeongezeka maradufu.

"Kila mtu ana sababu yake, lakini safari hii ongezeko ni kubwa zaidi ya miaka yote," alisema.

### KAULI YA LATRA

Uongozi wa LATRA umethibitisha Nipashe kuwa wimbi la wasafiri kwa sasa ni kubwa kuliko kawaida, hata kuilazimu mamlaka hiyo kutoa vibali maalum kwa mabasi ya ziada.

Umesema ongezeko kubwa la abiria wanaoondoka Dar es Salaam kwenda mikoani, lilianza kushuhudiwa Novemba 30 hadi jana, hatua iliyolazimu mamlaka hiyo kuruhusu mabasi zaidi kuingia barabarani ili kukidhi mahitaji.

Akizungumza katika Kituo cha Mabasi cha Magufuli-Mbezi jana, Ofisa Mfawidhi wa LATRA, Rukia Kibwana, alisema ongezeko hilo limekuwa kubwa kuliko kipindi chochote cha kawaida, hivyo kuhitaji suluhu ya haraka ili kuepusha usumbufu kwa wasafiri.

**"Wengine wameapa kuwa watakaoandamana wasithubutu kufika kwenye maeneo yao. Hayo yote yanaashiria wazi dhamira ya kuleta madhara makubwa,"**



DCP, David Misime

"Ni kweli, tangu Novemba 30 mpaka leo (jana), idadi ya wanaosafiri imekuwa kubwa sana. Tumeamua kuwaruhusu wasafirishaji wenye leseni hai, madereva waliothibitishwa, wanaotumia i-Button na ving'amuzi vya kufuatilia mwenendo wa magari, waombe vibali vya kuongeza magari katika mikoa yenye uhitaji mkubwa," alisema Rukia.

Aliongeza kuwa usafiri wa reli umekuwa mkombozi mkubwa, ukipunguza mzigo kwa mabasi na kusaidia kusafirisha abiria wengi hasa katika mikoa inayohudumiwa na usafiri huo.

### ULINZI MKALI

Kukiwa na hali hiyo, Nipashe pia imeshuhudia Jiji la Dar es Salaam likiingia katika wiki ya tahadhari, baada ya vyombo vya ulinzi na usalama kuimarisha ulinzi kwa kiwango ambacho hakijazoeleka, kufuatia madai ya maandamano yanayoratibiwa kuelekea Desemba 9.

Tangu Desemba Mosi, askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) na Jeshi la Polisi wameshuhudiwa wakitanda katika maeneo mbalimbali, wakiwa na silaha, magari ya doria na vifaa vingine vya kufanikisha ulinzi wa raia na mali zao.

Katika Barabara ya Bagamoyo, mojawapo ya barabara zenye shughuli nyingi zaidi, Nipashe imeshuhudia kuwapo askari wengi katika vituo kadhaa.

Katika eneo la Mwenge, askari wa JWTZ na Polisi walionekana wakiwa katika doria za pamoja, hali iliyoleta utulivu lakini pia maswali kwa wananchi.

Hali kama hii imeripotiwa pia katika maeneo ya Mbezi Beach Samaki, Africana, Tegeta kwa Ndevu, Tegeta Kibo, Boko Magengeni, Bunju A - Mianzini, Bamaga, Sayansi, Ubungo, Tabata Relini, Segerea - Mbuyuni, na kwenye Jengo la Mawasiliano, lililoko karibu na Mlimani City.

Kwa wengi, hali hiyo inakumbusha baa la Oktoba 29, wakati ghasia zilisababisha uharibifu wa mali, miundombinu na kusababisha Jeshi la Polisi kutoa amri ya watu kukaa ndani kwa muda ili kutuliza machafuko.

### KAULI YA RAIS

Akihutubia wazee wa Dar es Salaam juzi, Rais Samia Suluhu Hassan alithibitisha kuwa serikali imechukua hatua zote muhimu kuhakikisha nchi inabaki salama.

"Serikali itahakikisha ulinzi unaimarishwa, kulinda nchi, raia na mali zao," alisema Rais Samia akisisitiza kuwa ulinzi haujaimarishwa kwa ajili ya Desemba 9 pekee bali wako imara siku zote.

### KAULI YA POLISI

Jeshi la Polisi limetoa tahadhari dhidi ya kile linachoita mfululizo wa mipango ya uhalifu mkubwa unaoratibiwa kupitia mitandao ya kijamii, ikiwamo wito wa kuanzisha "maandamano ya amani yasiyo na kikomo" kuanzia Desemba 9, 2025.

Limesema mpango huo ni tishio kwa usalama wa wananchi, uchumi wa nchi na ustawi wa jamii.

Katika taarifa iliyotolewa jana, Msemaji wa Jeshi hilo, Naibu Kamishna wa Polisi (DCP) David Misime, alisema uchunguzi unaoendelea umebaini makundi mbalimbali mtandaoni yanayohamasisha vitendo vinavyoweza kusababisha vurugu kubwa na kusimamisha shughuli muhimu za kitaifa.

Alisema maandalizi hayo si ya amani kama yanavyodaiwa, kwani baadhi ya wahamasishaji wanatoa maelekezo ya matumizi ya silaha, wakisisitiza kuwa waliofunzwa pekee ndiyo wazitumie, jambo linaloashiria kuwapo silaha kwenye mpango huo.

DCP Misime alisema makundi hayo yanahamasisha kusimamisha shughuli zote za kiuchumi, kuharibu minara ya mawasiliano ili kukatiza huduma za mawasiliano nchini, na kuzuia shughuli za Bandari ya Dar es Salaam kwa kufunga barabara zote zinazoingia na kutoka bandarini.

Ujumbe mwingine unaosambazwa mitandaoni, alisema, unawahimiza waandamanaji kufunga mipaka ya nchi, kupora mali, kuvamia hospitali na kuzizuia kutoa huduma, vitendo ambavyo alisema ni hatari kwa maisha ya watu na kwa uchumi.

"Wengine wameapa kuwa watakaoandamana wasithubutu kufika kwenye maeneo yao. Hayo yote yanaashiria wazi dhamira ya kuleta madhara makubwa," alisema.

DCP Misime alisisitiza kuwa maandamano yasiyo na kikomo ni kinyume cha haki, kwani yanawazuia wengine kufanya shughuli halali za kujipatia kipato.

"Ukinizuia kutoka kutafuta riziki unavunja haki zangu na kunihatarishia maisha," alisema DCP Misime akinukuu moja ya kauli za makundi yanayosigana kati ya wahamasishaji maandamano na wanaopinga maandamano hayo.

Jeshi la Polisi limeutaja mkakati huo kama uhalifu mkubwa unaoendelea kuhamasishwa, likitoa wito kwa wananchi kuwakataa wahamasishaji wa vurugu na kulinda amani ya Taifa, hasa ikizingatiwa majeraha ya kijamii yaliyotokana na matukio ya Oktoba 29 na siku zilizofuata.

Vilevile, wananchi wamehimizwa kuendelea na maandalizi ya sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya kwa kuzingatia usalama wa maisha na mali zao, kuhakikisha makazi yao yanakuwa na uangalizi wanaposafiri na kufuata sheria za usalama barabarani ili kuepuka ajali.

***Imeandikwa na Elizabeth Zaya, Halfani Chusi na Romana Malya**

CamScanner